



GRETCHEN WHITMER
GOVERNOR

STATE OF MICHIGAN
OFFICE OF THE GOVERNOR
LANSING

GARLIN GILCHRIST II
LT. GOVERNOR

AGIZO LA UTENDAJI

No. 2020-13

Nyongeza za muda kwa uwezo wa kufanya kazi na ufanisi wa vituo vya utunzaji wa afya

Virusi vya corona (COVID-19) ni virusi vinavyoleta ugonjwa wa kupumua ambayo inaweza kusababisha maumivu mengi au hata kifo. Husababishwa na aina mpya ya virusi vya corona vinavyopatikana kwa wanadamu na ni rahisi kuenea kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Mpaka sasa hakuna chanjo au matibabu ya ugonjwa huu.

Mwezi wa Tatu, tarehe 10, mwaka wa 2020, Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Michigan ilitambua kesi mbili zilizobainika kuwa na maambukizi ya CORONA-19 hapa Michigan. Siku hiyo hiyo, nilitoa agizo la Utendaji 2020-4. Agizo hili lilitangaza hali ya hatari katiko jimbo lote chini ya sehemu 1 cha kifungu cha 5 cha Katiba ya Michigan ya 1963, Sheria ya Usimamizi wa Dharura, 1976 PA 390, kama ilivyorekebishwa, MCL 30.401-.421, na Nguvu za Dharura za Gavana 1945, 1945 PA 302, kama ilivyorekebishwa, MCL 10.31-.33.

Sheria ya Usimamizi wa Dharura inampa gavana nguvu yenye upana na majukumu ya “kukabiliana na hatari serikalini na watu wa serikali husika itakayotokana na janga au dharura”, sheria hiyo ambayo gavana ataitekeleza kupitia “agizo la mtendaji”, matangazo, na maagizo yenye athari na nguvu kisheria.” MCL 30.403(1)-2. Vile vile nguvu ya kisheria ya gavana ya mwaka 1945, inasema kwamba, baada ya kutangaza hali ya dharura, “gavana anaweza kutangaza maagizo, kupitia kanuni na sheria inayofaa kwa ulazima wa kulinda maisha na mali au kuweza kusaidia hali ya dharura kutulia.” MCL 10.31(1)

Kwa sababu ya kutoa usalama kutokana na hatari la hili jimbo kutokana na janga la COVID-19, lazima hili jimbo lihakikishe ya kuwa kuna usambazaji wa kutosha wa watoa huduma za afya na vituo vya afya vinafyohitajika. Kwa hili sababu, ni sahihi na lazima kutoa msaada mdogo na wa muda kutoka mahitaji fulani ya kisheria ili kuogeza uwezo wa kufanya kazi na ufanisi wa vifaa vya afya.

Kwa kupitia katiba ya Michigan ya 1963 na sheria ya Michigan, ninaamuru yafuatayo:

1. Kwa uzingativu wa mara moja na kuendelea hadi kufikia Aprili 14, 2020 saa 11:59 jioni, Idara ya Afya na Huduma za Binadamu (“DHHS”) inaweza kutoa cheti cha darura cha hitaji la mwombaji kazi na kuahirisha kufuata kwa ukamilifu majitaji na utaratibu yafuatwayo kwa kawaida katika kifungu 22235 cha Msimo wa Afya ya Umma, 1978 PA 368, kama ilivyorekebishwa, MCL 333.22235, hadi kukomesha hali ya dharura chini ya kifungu cha 3 cha Utendaji 2020-4.
2. Kwa uzingativu wa mara moja na kuendelea hadi kufikia Aprili 14, 2020 saa 11:59 jioni, Idara ya Leseni na Mambo ya Udhhibiti (“LARA”) inaweza kutoa kiboreshaji chini ya kifungu cha 21564 cha Msimbo wa Afya ya Umma, 1978 PA 368, kama ilivyorekebishwa, MCL 333.21564, kwa hospitali yoyote yenye leseni katika jimbo hili, bila kujali idadi ya vitanda au eneo, kwa kusudi la kutoa utunzaji wakati wa dharura ya COVID-19, kujenga, kupata, au kuendesha kituo cha muda au cha rununu kwa madhumuni yoyote ya utunzaji wa afya, bila kujali mahali kituo iko.
3. Kwa uzingativu wa mara moja na kuendelea hadi kufikia Aprili 14, 2020 saa 11:59 jioni, Idara ya LARA inaweza kutoa usajili wa muda kwa mwombaji kazi kama msaidizi wa muuguzi aliyethibitishwa, bila kujali kama mwombaji anaonyesha LARA kwamba amekamilisha mahitaji ya uchunguzi wa sehemu 21911 na 21913 ya Msimbo wa Afya ya Umma, 1978 PA 368, kama ilivyobadilishwa, MCL 333.21911 na MCL 333.21913. Usajili wa muda mfupi uliotolewa chini ya kifungu hiki itakuwa halali kwa siku 28 na inaweza kufanywa upya na LARA hadi kukomesha kwa hali ya dharura chini ya kifungu cha 3 cha Agizo la Utendaji 2020-4.
4. Kwa uzingativu wa mara moja na kuendelea hadi kufikia Aprili 14, 2020 saa 11:59 jioni, Idara ya LARA inaweza kurekebisha leseni ya kufanya mazoezi chini ya Sehemu ya 170, 172, 175, 177, au 187 ya Nambari ya Afya ya Umma, 1978 PA 368, kama ilivyorekebishwa, bila kujali ikiwa mwenye leseni amekidhi mahitaji ya kuendelea ya masomo yanayotumika kwa leseni yao.
5. Kwa uzingativu wa mara moja na kuendelea hadi kufikia Aprili 14, 2020 saa 11:59 jioni, Idara ya LARA inaweza kutambua masaa ya mfanyikazi kwa kazi ya kujibu dharura ya COVID-19 kama masaa yanayohesabika kama kwamba mfanyikazki ameendelea na masomo au programu zinazohitajika kwa kupewa leseni.
6. Kwa uzingativu wa mara moja na kuendelea hadi kufikia Aprili 14, 2020 saa 11:59 jioni, Idara ya LARA inaweza kumruhusu msaidizi ambaye sio muuguzi kama mratibu wa shughuli, mfanyakazi wa jamii, au anayetitolea kusaidia kumlisha au kumsafirisha mgonjwa au mkazi kwa njia inayolingana na mpango wa utunzaji wa mgonjwa au mkazi.

Imetolewa kwa idhini wa mkono wangu na Muhuri Mkuu wa Jimbo la Michigan

Tarehe: Machi 17, 2020

Wakati: 5:59 jioni


GRETCHEN WHITMER
GAVANA

Na Gavana:

KATIBU WA SERIKALI